

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA

IMEIDHINISHWA KWA KIWANGO CHA ISO 9001:2015



TAARIFA KWA UMMA

KIKAO CHA WADAU CHA KUJADILI NA KUPITIA RASIMU ZA KANUNI MPYA NA ZILIZOFANYIWA MAREKEBISHO ZA USAFIRI WA ANGA ZA MWAKA 2026

Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Uchukuzi, inawaalika wadau wa sekta ya usafiri wa anga na wananchi wote kwa jumla kushiriki katika kikao cha wadau cha kujadili na kupitia Rasimu za Kanuni Mpya na Zilizofanyiwa Marekebisho za Usafiri wa Anga za Mwaka 2026. Lengo la kikao hicho ni kupokea maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu rasimu za Kanuni kabla ya kukamilishwa, kwa lengo la kuimarisha usalama (safety), ulinzi (security), ufanisi na maendeleo endelevu ya sekta ya usafiri wa anga nchini.

Kikao cha wadau kitafanyika tarehe 9 hadi 10 Julai 2026 saa 2 asubuhi katika Ukumbi wa Mikutano wa Alpha, Makao Makuu ya TCAA, Aviation House, Makutano ya Barabara za Nyerere na Kitunda, Banana, Ukonga, Dar es Salaam.

Rasimu za Kanuni zitakazojadiliwa ni:

- a) The Civil Aviation (Remotely Piloted Aircraft) Regulations, 2026;
- b) The Civil Aviation (Aeronautical Radio Frequency Spectrum Utilization) (Amendment) Regulations, 2026;
- c) The Civil Aviation (Heliports) Regulations, 2026;
- d) The Civil Aviation (Operation of Aircraft – Commercial Air Transport) (Amendment) Regulations, 2026;
- e) The Civil Aviation (Personnel Licensing) (Amendment) Regulations, 2026;
- f) The Civil Aviation (Ground Handling Services) Regulations, 2026;
- g) The Civil Aviation (Safety Management System) (Amendment) Regulations, 2026;
- h) The Civil Aviation (Radio Navigation Aids) (Amendment) Regulations, 2026;
- i) The Civil Aviation (Security) (Amendment) Regulations, 2026;
- j) The Civil Aviation (Communication Systems and Procedures Relating to Remotely Piloted Aircraft Systems C2 Link) Regulations, 2026. na
- k) The Civil Aviation (Meteorological Service for Air Navigation) Regulations, 2026

Rasimu za Kanuni, Ratiba ya Mashauriano ya Wadau pamoja na Fomu ya kutolea maoni zinapatikana kupitia tovuti yetu www.tcaa.go.tz.

Wadau wanahimizwa kupitia rasimu za Kanuni na kuwasilisha maoni yao kwa kutumia Fomu ya kutolea maoni iliyoambatishwa kupitia barua pepe dg@tcaa.go.tz, nakala zikitumwa pia kwa deus.nkambaulaya@tcaa.go.tz na karen.luoga@tcaa.go.tz, kabla au ifikapo tarehe 10 Julai 2026.

TCAA inawahimiza wadau wote wa sekta ya usafiri wa anga na wananchi wote kwa jumla kushiriki kikamilifu katika kikao hiki na kutoa maoni yao ili kuchangia uboreshaji wa mfumo wa kanuni za usafiri wa anga nchini.

Imetolewa tarehe Juni 27, 2026.



Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Sat Jun 27 13:26:59 EAT 2026

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU